KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na Randy Maxwell (Mchungaji wa Renton SDA Church, Washington)

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

JUMA LA TANO: APRILI 23 – APRILI 30, 2020

"MBINGU DAIMA IKO WAZI"

Jumapili kadhaa zilizopita, Suzette na mimi tulikuwa tumechoka kubaki tumefungiwa ndani ya nyumba, kwa hiyo tuliamua kuendesha gari kwenda *The Landing* – soko kubwa la nje, kule Renton jijini Washington, mahali tunapoishi ambapo pana maduka, migahawa, huduma mbali mbali na ukumbi wa sinema.

Duka la miwani nililodhamiria kutembelea lilikuwa na bango mlangoni lililokuwa linasema, kwa sababu ya COVID-19 limefungwa hadi itakapotagazwa tena. Lakini lile halikuwa ndio duka pekee. Tulizunguka hadi duka liitwalo Rosss, nalo lilikuwa limefungwa. Duka la vifaa vya michezo liitwalo Dick-limefungwa. Duka la Marshall-limefungwa. World Market – limefungwa. Eneo la maegesho lilikuwa ni mji hewa. Kirusi kisichoonekana kililuwa kinaonesha nguvu yake kuyafanya magari na wanunuzi watoweke.

Siku chache kabla, Gavana Jay Inslee, alikuwa ametoa amri ya watu kubaki ndani ya nyumba, amri hiyo kimsingi ilipelekea kulifunga jimbo zima la Washington. Kwa hiyo ni katika mantiki hiyo, ninaandika somo hili. Ndio maana ninalikubali tukio la Yesu alipokutana na mtafuta ukweli mwenye mashaka aitwaye Nathanaeli.

Yesu alikuwa akielekea Galilaya. Akiwa njiani alimwambia Filipo amfuate. Kisha Filipo akaenda kumtafuta rafiki yake, Nathanaeli, na kumwambia, "Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti." Yohana 1:45.

Kutajwa kwa Nazareti kulichochea mwitikio ndani ya Nathanaeli kama watu leo wanaposikia Coronavirus ikitajwa. Coronavirus imefunga mambo yote. "Nazareti! Laweza neno jema kutoka Nazareti? Nathanaeli aliuliza. Tunaweza kuuliza, kuna kitu cho chote kinaweza kutoka kwenye hii coronavirus? Kutokana na usumbufu na ugumu wa kujitenga na jamii? Kutoka kwenye makusanyiko yanayoshindwa kukutana kwenye nyumba zao za ibada? Lakini, nyakati fulani mambo mazuri hutoka kwenye sehemu mbaya au kwenye uzoefu mbaya.

Pongezi kwa Nathanaeli, aliitikia mwaliko wa Filipo uliosema, "njoo uone" akaenda naye. Yesu alimwona Nathanaeli akija akasema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli, hana hila ndani yake."

"Umepataje kunitambua? Aliuliza Nathanaeli. Yesu akajibu, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini nilikuona" Yohana1:48. Ghafla, imani ikafungua moyo wa Nathanaeli uliokuwa umefungwa na akaungama: Rabi, wewe u mwana wa Mungu, ndiwe mfalme wa Israeli. (f. 49)

Yesu akajibu, akamwambia, Kwa sababu nilikuambia, Nilikuona chini ya mtini, waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya. Akamwambia, Amin, amin, nawaambia, Mtaziona mbingu zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu. (f. 50, 51)

Wakati wa ubatizo wa Yesu, "mbingu zilifunguka," na Mungu alimtia mafuta na kumbariki mwanae kwa maneno. (Soma Mt. 3:16-17) Kristo kwa hakika anasema, "Kwenye kingo za mto Yordani mbingu zilifunguka, Roho alishuka kama hua juu yangu. Ile ilikuwa ni ishara kuonesha

kuwa mimi ni mwana wa Mungu. Kama mwaniamini mimi, imani yenu itaimarishwa. Mtaona mbingu zikifunguka na hazitafungwa kamwe. Nimezifungua kwa ajili yenu. Malaika wa mbinguni wanapanda, wapeleka juu kwa Baba maombi ya wenye mahitaji na wenye dhiki, na wanashuka wakileta baraka na tumaini, kuwatia moyo, kuwapa msaada, na uzima watoto wa wanadamu.'" (*Desire of Ages*, p. 142, 143)

Haleluya! Mbingu iko wazi. Mbingu daima iko wazi, na hakuna ubaguzi, wala mashaka, au COVID-19, au amri ya zuio la kubakia nyumbani, au mashetani, iwe kimo au kina, wala kitu kingine cho chote katika viumbe vyote kinachoweza kufunga milango ya mbingu. (Soma Rum. 8:39.) Na inamaanisha nini mbingu kuwa wazi? Ina maana kuwa mimi na wewe tuna ruhusa kamili wa kupata kila kitu kilichoko pale, na "rafu" (shelves) daima zimesheheni kila tunachohitaji.

Ni nini kilichohifadhiwa mbinguni?

- Kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya maisha na wema (2 Pet. 1:3).
- Tunda la Roho (Wagalatia 5:22, 23).
- Silaha za Mungu (Waefeso 6:14-17).
- Ahadi kuu kupita kiasi na za thamani (2 Pet.1:4).
- Kuzaliwa upya katika tumaini lililo hai (1Pet. 1:3-5).
- Nia ya Kristo (1 Kor. 2:16).
- Kila baraka ya kiroho katika Kristo (Waefeso 1:3).

Mbingu iko wazi na Yesu ametupatia ufunguo wa ufalme (Mt. 16:19). Ufunguo huo ni maombi. Malaika ni kama mawakala wanaosambaza bidhaa, wanapeleka maombi yetu juu kwa Baba na wanaposhuka, wanaleta mibaraka tunayoihitaji zaidi, yaani tumaini, kutiwa moyo, msaada, na uzima.

Duka la *The Landing* linaweza kuwa limefungwa, duka la vifaa vya michezo linaweza kuwa limefungwa, migahawa yaweza kuwa imefungwa, hata makanisa yetu yanaweza kuwa yamefungwa kwa muda, lakini MBINGU DAIMA IKO WAZI. Kwa hiyo, usiogope. Yesu anasema, "Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya" Yohana 14:14. Kwa hiyo, "Fumbua sana kinywa chako nami nitakijaza" Zaburi 81:10.

Hiki kirusi cha corona hakiwezi kumzuia Mungu. Omba kuliko ilivyokuwa kabla, kwa sababu MBINGU DAIMA IKO WAZI.

Maswali ya Moyoni: Je! Makabati yako ya kiroho yako wazi katika baadhi ya vyumba kwa sababu ya shughuli nyingi na haraka za maisha katika miaka hii michache ya mwisho? Inawezekana kuna baadhi ya mahitaji ya mbinguni na neema unazohitaji kuwa nazo kama akiba? Zaidi sana, endapo utaomba karama yo yote ya kiroho, ushindi katika eneo lo lote, au baraka zingine za kiroho, ungeomba kitu gani? Yafikirie maswali haya kwa dakika chache.

Chagamoto hai za Moyoni: Kwa nini usitumie muda kuorodhesha mambao unayohisi kuwa unayahitaji juma hili – kisha utafute kwenye Biblia ahadi mahsusi ambapo Mungu anatuambia kuwa atatupatia hilo hitaji. Iwe ni fedha kwa ajili ya kulipa bili, au nguvu katika eneo ambalo umekuwa dhaifu kiroho, unapoomba anza kudai kwa vitendo ahadi za Mungu.

"Haikupasi kwenda kwenye miisho ya dunia kwa ajili ya kutafuta hekima, kwani Mungu yupo karibu. Sio uwezo ulionao sasa au utakao kuwa nao baadaye utakaokupatia mafanikio. Tunahitaji kuwa na tumaini kidogo juu ya kile mwanadamu anachoweza kufanya na kuwa na tumaini zaidi juu ya kile Mungu anachoweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini. Anatamani umwendee kwa imani. Anatamani wewe utarajie mambo makubwa kutoka kwake" (COL. 146)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hil

- Ellen White, *Steps to Christ*, chapter 11, "The Privilege of Prayer" - Attached
- Randy Maxwell, *Boot Camp for the Last Days*

Siku ya 29, Ijumaa, Aprili 24, 2020

Taarifa ya Sifa: Idara ya Vijana katika Divisheni ya Euro-Asia kule Moscow, Urusi, hivi karibuni iliandaa programu ya maombi kwa divisheni nzima kwa ajili ya vijana kwa njia ya mtandao wa Zoom. Walioshiriki waliungana kwa pamoja divisheni nzima wakilenga nguvu ya Mungu, ulinzi wake, na maombi. Mungu alibariki!

MAMBO YA KUOMBEA

- Omba kwamba vijana wetu kote ulimwenguni waendelee kushikamana katika maombi na kujifunza Biblia. Omba ili uzoefu wanaoupata sasa pamoja na Yesu uweze kudumu.
- Ombea wazazi wanaohangaika kuwafundisha au kuwasaidia watoto wao kufuatilia elimu inayotolewa kwa njia ya mtandao wakati wa janga hili. Ombea wazazi wawe na hekima na watiwe moyo.
- Ombea wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita na vyuo ambao watakosa mahafali yao. Ombea watiwe moyo, na wapate mwelekeo wa mipango yao ya baadaye.
- Ombea afya, nguvu, na uvuvio kwa viongozi wa huduma za vijana, na wengine wanaofanya kazi ya kuwatia moyo vijana wetu wakati wa zahama hii.
- Ombea mikutano ya injili iitwayo, “Awakening Hope” inayoendeshwa na *It Is Written* kwa njia ya mtandao ambayo imeanza hivi karibuni. Kumekuwa na vikwazo vingi sana na tunajua kuwa adui amekuwa akizuia kadiri muda unavyokwenda ili hii programu isisonge mbele. Dumisha maombi kwa ajili ya mikutano hii. Pia tembelea:https://www.discoverhopeawakens.com

Siku ya 30, Jumamosi, Aprili 25, 2020

OMBA KWA MAPENZI YA MUNGU

“Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia.” 1 Yohana 5:14

“Katika ombi la imani kuna sayansi ya kimbingu; ni sayansi ambayo kila mmoja anayetaka maisha yake yafanikiwe ni lazima aifahamu. Kristo anasema, “Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu” Marko 11:24. Anaweka wazi kwamba maombi yetu ni lazima yawe kwa mapenzi ya Mungu; inatupasa kuomba mambo aliyoahidi, na kila tunayopokea ni lazima yatumike kufanya mapenzi yake. Masharti yakitimizwa, ahadi zitatimizwa… hatuhitaji kutafuta ushahidi wa nje kwa ajili ya baraka. Kipawa kipo ndani ya ahadi, na tunaweza kuendelea na kazi yetu tukiwa na hakika kuwa kile alichoahidi Mungu anaweza kutenda, na kwamba kipawa tulichonacho tayari, kitaonekana pale tunapokihitaji zaidi” *Education*, p. 258

Maswali ya Moyoni: Je! Umewahi kuomba kitu fulani ambacho ulijua kuwa sio mapenzi ya Mungu, lakini ulikihitaji sana, uliendelea kuomba hivyo hivyo? Mara nyingi yaliyopita ni bora kuliko yajayo. Kwa nini usitumie muda kidogo leo kutafakari mambo ya nyuma na kumshukuru Mungu kwa yale maombi mahsusi ambayo hakuyajibu, kwa sababu sasa unagundua kwamba yalikuwa hayana faida kwako.

Taarifa ya sifa: Ingawa tumewapoteza wapendwa wetu kwa COVID-19, wapo wengine ambao tumewaombea kwa dhati na Mungu amehifadhi uhai wao. Hebu tumshukuru kwa ajili ya matukio ambapo Mungu ameokoa. Na hebu tutafute kushilikilia “Tumaini Letu Lenye Baraka” tunapoendelea kumtumaini hata katika hasara tusizozielewa.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea watu wa maeneo ya Chattanooga, Tennessee kule Marekani, ambao hivi karibuni walikumbwa na tufani za kutisha. Wengi walipoteza makazi yao na wengine maisha yao, na sasa katikati ya janga la COVID-19 wanahangaika namna ya kutengeneza yaliyoharibika.
- Ombea walio kwenye nchi fukara ambao wamekuwa hawana uwezo wa kufanya kazi. Ombea wapate chakula na mahitaji ya washiriki wa kanisa katika maeneo hayo.
- Endelea kuwaombea wataalamu wa afya walio mstari wa mbele wanaoendelea kupambana na janga hili. Ombea usalama wa afya zao, usalama wa hisia zao wanapoendelea kushughulika na watu wenye misongo itokanayo na janga hili.
- Endelea kuombea taasisi, na biashara ndogo ndogo zinazokumbwa na uhaba wa kifedha kwa sababu ya watu kufungiwa. Ombea ipatikane hekima ya namna ya kusonga mbele.
- Ombea viongozi wapate hekima ili wajue namna na ni wakati gani wa kuanza kufungua mambo tena kwa ajili ya uchumi.
-

Siku ya 31, Jumapili, Aprili 26, 2020

OMBA KISHA SUBIRI MBINGU ZITENDE

“Nami nitamwita Mungu, Na Bwana ataniokoa; Jioni, asubuhi, na adhuhuri nitalalama na kuugua, Naye ataisikia sauti yangu. Ameiokoa nafsi yangu iwe salama, asinikaribie mtu, Maana walioshindana nami walikuwa wengi” zaburi 55:16-18.

“Maombi ni njia iliyowekwa na mbingu kwa ajili ya mafanikio. Rufaa, maombi, maombezi, kati ya mtu na mtu, huwagusa watu na huwa na sehemu katika kudhibiti mambo ya mataifa. Lakini, maombi hugusa mbingu... maombi, imani, kumtumainia Mungu, huleta uweza wa kimbingu, ambao huiweka mipangilio ya kibinadamu katika hali halisi ya kutostahili. Mtu ambaye hujiweka kwenye nafasi ambayo Mungu atamwangazia, husonga mbele, kana kwamba anatoka kwenye giza la utusitusi hadi kwenye nuru kamili ya mchana.” *In Heavenly Places*, p. 75

Maswali ya Moyoni: Ni jambo gani lisilowezekana zaidi ambalo unaomba Mungu alifanye? Je! Ni kuleta upatanisho kati yako na mtu fulani umpedaye? Je! Ni kurejesha ndoa iliyovunjika, au kuwarudisha watoto kwenye imani? Leo orodhesha maombi kadhaa yasiyowezekana moyoni mwako, na kando ya maombi hayo, andika ahadi mahsusi za Mungu kutoka katika neno la Mungu. Anza kwa kudai ahadi zifuatazo: Marko 10:27, Luka 18:27, 1 Yohama 5:14

Taarifa ya Sifa: Tunamshukuru Mungu kwa vile tayari amekwishalitumia janga la COVID-19 kuleta upatanisho kati ya watu wengi, na tunajua kuwa Mungu anatamani kutenda mujiza sawa na huo kwa ajili ya kuwaponya wengi zaidi.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea washiriki wa kanisa katika Afrika, visiwa vya Karibeani, nchi za Amerika ya kati na kusini wanapoendelea kupambana na janga coronavirus.
- Ombea wale ambao wako ndani ya jumuia ya kanisa lako na wamekumbwa na zahama ya kiuchumi. Omba ili mahitaji yao yapatikane.
- Ombea moyo wa ukarimu kwa wale wenye rasilimali za ziada. Ombea kwamba sisi kama kanisa tuungane kuwasaidia ndugu na dada zetu wenye mahitaji.
- Omba kwamba Mungu atufanye tuwe na muda pamoja naye kwa ibada ya kina, sio tu kwa ajili ya kupata msaada na kupokea baraka, bali kwamba shauku yetu kuu iwe ni kumjua kweli kweli.
- Omba kwamba washiriki wa kanisa ulimwenguni kote watumie fursa hii kwa dhati katika kuwapatia marafiki na majirani masomo yanayotolewa na *It Is Written* kwenye mikutano ya “Hope Awakens” au chakula kingine cha kiroho wanachohitaji.

Siku ya 32, Jumatatu, Aprili 27,2020

DAI AHADI

“Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa” (2 Pet. 1:3-4).

“Kila ahadi iliyo ndani ya Neno la Mungu ni kwa ajili yetu. Katika maombi yako, wasilisha neno alilosema Yehova na kwa imani dai ahadi zake. Neno lake ni uhakikisho kwamba ikiwa utaomba kwa imani, utapokea baraka zote za kiroho. Endelea kuomba, na utapokea kwa uwingi kuliko unavyoomba au kufikiri. Jielimishe kuwa na tumaini lisilo na mipaka kwa Mungu. Mtwike fadhaa zako zote. Mngoje kwa uvumilivu na ataliepusha.” *In Heavenly Places*, p. 71

Maswali ya Moyoni: Kuwa na tumaini lisilo na mipaka kwa Mungu na Neno lake ina maanisha nini? Ikiwa kila ahadi iliyo ndani ya Neno la Mungu ni kwa ajili yetu, kama tulivyoambiwa, ni kwa nini bado tunasita-sita kuliamini Neno lake? Ni kwa njia gani ambazo tunaweza kubadilisha maombi yetu yenye mashaka na kuyafanya yawe ni maombi yenye imani yenye tumaini? (Soma: Yohana 6:37, Ebr. 11:6, na Rum. 10:17)

Taarifa ya Sifa: Tunamsifu Mungu kwa kufanikisha masuala ya kiufundi ya mkutano wa injili wa “Hope Awakens” inayoendeshwa na *It Is Written*. Tunaendelea kuomba ili Mungu atupatie mahitaji na ulinzi kwa ajili ya mfululizo.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wale ambao kwa sasa wanaendelea kusikiliza na kutazama mfululizo wa mikutano ya “Hope Awakens” chini ya *It is Written*. Omba kwamba mioyo mingi na maisha ya wengi yabadilishwe milele.
- Ombea wale wanaoendelea kupambana na COVID-19. Omba ili Mungu awapatie pumzi ya uponyaji wa kimwili na kiroho.
- Tuwaombee watendakazi walio mstari wa mbele kutoa huduma muhimu kama vile, afya, wafanyakazi wa maduka, na huduma za kusambaza bidhaa. Omba ili mkono wa ulinzi wa Bwana uwe juu yao wanapoendele na kuwahudumia wengine na kudumisha huduma zao muhimu.
- Ombea wazee ambao wamekwama kwenye nyumba za malezi ya wazee ambamo familia zao haziwezi kuwatembelea. Wengine hawawezi kuelewa ni kwa nini hali iko hivi. Omba kwamba neema za Mungu za zinazotegemeza ziwe juu yao.
- Omba kwa ajili ya wale wanaosumbuka kwa msongo, hofu, na hasa wale wanaoishi peke yao. Kama unamjua mtu mwenye changamoto hizi, omba upate njia za kumfikia na kumwonesha kujali, kwa njia za kijamii zilizo salama na za kufaa.

Siku ya 33, Jumanne, Aprili 28, 2020

OMBA KUFUNGULIWA

“Nalimtafuta Bwana akanijibu, Akaniponya na hofu zangu zote. Wakamwelekea macho wakatiwa nuru, Wala nyuso zao hazitaona haya. Maskini huyu aliita, Bwana akasikia, Akamwokoa na taabu zake zote. Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa.” (Zab. 34:4-7)

“Tuna imani kidogo mno. Tunamwekea mipaka Mtakatifu wa Israeli. Inatupasa tumshukuru Mungu kwani huridhika kumtumia ye yote kati yetu kama chombo chake. Kwa kila ombi la dhati lililoombwa kwa imani kwa ajili ya jambo lo lote, majibu yatatolewa. Majibu yanaweza yasije kama yalivyotarajiwa; lakini yatakuja – huenda sio kama tulivyopanga, lakini yatakuja kwa muda tunapoyahitaji zaidi.” *Gospel Workers*, p. 92

Maswali ya Moyoni: Huenda unapoitazama jamii yako unawaona baadhi ya watu ambao wanachechemea katika imani zao. Kwa nini usifikirie kuhusu njia za kivitendo za kushiriki imani pamoja na kaka au dada mwenye hitaji. Labda mshirikishe kitabu kizuri (au mpendekezee kitabu kizuri) kinachojenga imani, kama vile “Njia Salama” au “Tumaini la Vizazi Vyote.” Tunapoona jinsi Mungu ambavyo amefanya miujiza katika maisha ya wengine, tunaweza kuwa na tumaini kwa maisha ya kesho. Au andika kadi yenye baadhi ya ahadi za Biblia na kumpatia mtu fulani mwenye hitaji. Ikiwa huna uhakika ni nani wa kumfikia, mwombe Mungu naye atakuonesha!

Taarifa ya sifa: Kule Ufilipino, kama matokeo ya hili janga, maelfu ya vijana wanaomba pamoja kila siku kwa mtandao wa Zoom, na mioyo mingi inavunjwa na kuvutwa kwa Yesu. Tunamsifu Mungu kwa kuwa roho ya maombi inakua kila mahali. Pia wengi wanatafuta uelewa wa kina wa Neno la Mungu

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea mchungaji mahalia. Omba ili Mungu amtegemeze, amlinde, na muhimu zaidi, ampatie ujazo wa Roho Mtakatifu kwa uwingi zaidi.

- Ombea uongozi wa kanisa wa Konferensi Kuu, watawala, na wakurugenzi wa idara na wafanyakazi wote. Omba ili Roho Mtakatifu awapatie hekima wanapotafuta kuongoza na kuhamasisha utume wa kanisa katika zahama hii.

- Omba mahsusi kwa ajili ya Ted Wilson, Mwenyekiti wa Konferensi Kuu, GT. Ng, Katibu, na Juan Prestol, Mhazini. Omba wawe na hekima maalum, ulinzi kwa familia zao, na baraka za Roho Mtakatifu wanapoendelea kuongoza katikati ya zahama hii.
- Omba uongozi wa Mungu kwa siku za usoni za kanisa letu. Omba kwamba tusiipoteze fursa ya kushiriki upendo wa Yesu na ukweli mzuri wa Ufunuo 14 na 18 kwa ulimwengu wenye hitaji.

- Omba kwa dhati ili Mvua ya Masika ishuke kama Mungu alivyoahidi, ili kazi imalizike na twende nyumbani. Muda huu sio wa kufanya kazi kama tulivyozoea. Ni wakati wa kumaliza kazi na kujitayarisha kumpokea Yesu.

Siku ya 34, Jumatano, Aprili 29, 2020

DAIMA OMBA KWA UNYENYEKEVU

"Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida. Nao wakujuao jina lako wakutumaini Wewe, Maana Wewe, Bwana hukuwaacha wakutafutao. Mwimbieni Bwana akaaye Sayuni, Yatangazeni kati ya watu matendo yake. Maana mlipiza kisasi cha damu awakumbuka, Hakukisahau kilio cha wanyonge." (Zab. 9:9-12)

"Ombi la dhati lililotolewa kutoka kwenye moyo ulioongoka, lililoombwa na na mtu anayetamani kufanya mapenzi ya Mwalimu Mkuu linathamani zaidi mbele za Mungu kuliko uwezo wa kuongea. Wakala wa kibinadamu anaweza asiwe na sauti kwenye mabaraza ya sheria, anaweza asiruhusiwe kuingia kwenye mijadala ya mabaraza ya uongozi au kupiga kura bungeni, lakini anaweza kumfikia Mungu. Mfalme wa wafalme huinama chini kusikiliza ombi litokalo kwenye moyo mnyenyekevu na wenye roba. Mungu husikia kila ombi linalotolewa kwa uvumba wa imani. Mtoto wa Mungu aliyedhaifu kabisa anaweza kuwa na mvuto wenye mwafaka na mabaraza ya mbinguni." *That I May Know Him*, p. 270

Maswali ya Moyoni: Kama mwandishi mmoja anavyosema, "Kiburi hakisikilizi, Kinajua tarari" Je! Yawezekana kwa njia fulani umeruhusu kiburi kuathiri mbinu zako za kusikiliza? Yawezekana kwa njia fulani umeruhusu kiburi kutawala ulimi wako, au hata kuongoza maombi yako? Kama ndiyo, omba kwamba Mungu akuoneshe namna ya kuwaomba msamaha wale uliowajeruhi kwa kuzungumza na kuishi kwako kwa kiburi. Hili ni gumu, lakini, ikiwa tunataka Mungu apokee maombi yetu, inatupasa kuweka pembeni kiburi kati yetu wenyewe na kwa namna ya pekee dhidi yake. Soma Yakobo 4:10, Isa. 57:15)

Taarifa ya Sifa: Tunamsfifu Mungu kwa vile Yeye anatawala dunia hii na bado amekaa kwenye kiti cha enzi. Ingawa kwa wengi wetu maisha yanaonekana kukosa udhibiti, tunaweza kupumzika katika usalama wa mikono yake aliyeahidi kwamba hatatupungukia wala hatatuacha kabisa. Kumbuka, Yeye aliliona hili janga lote la COVID-19 kabla halijaja juu ya ulimwengu, na hakuna kitu hutugusa sisi hadi Yeye aruhusu. Kwa hiyo, kama tunahangaika na ugonjwa, hasara za kifedha, au mitihani mingine na maumivu – hebu tumsifu Mungu kwani bado yupo kwenye kiti cha enzi na jambo ambalo adui analikusudia kwa mabaya, Mungu anaweza kuligeuza kuwa jema.

MAMBO YA KKUOMBEA

- Omba kwa wale ambao kwa namna ya pekee hawana sauti kwa ajili ya kupambana wao wenyewe au kupata msaada wakati wa zahama hii.
- Ombea watoto, wazee, walio udhaifu, akina mama wanaoishi peke yao wakihangaika kujikimu.
- Ombea idadi ya ya wakimbizi waliowekwa kwenye makambi kule Ulaya, Ugiriki na nchi zingine duniani. Ombea wapate mahitaji yao ya afya na haki zao kama wanadamu kusaidiwa.
- Endelea kuomba kwa ajili ya wamishonari wengi ambao wamezuiliwa kwenye vituo vyao vya kazi katika maeneo mbali mbali ulimwenguni. Ombea mahitaji yao ya kimwili na kiusalama.
  Ombea wale waliopona kutokana na coronavirus waendelee kupata nguvu na urejeshwaji wa afya zao. Ombea uponyaji wa mapafu, na nguvu za kurejea kwenye maisha ya kawaida.

Siku ya 35, Alhamisi, Aprili 30, 2020

OMBA NEEMA YAKE

“Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.” 2 Kor. 12:9-10

“Mungu atafanya mambo makubwa kwa wale wanaomtumainia. Sababu kwa nini watu wanaomkiri hawana nguvu kubwa ni kwamba wanatumainia zaidi hekima yao wenyewe, na hawampi Bwana fursa ya kudhihirisha uweza wake kwa niaba yao. Katika kila dharura atawasaidia watoto wake wanaoamini ikiwa wataweka tumaini lao lote kwake na kumtii kwa uaminifu.” *Patriarchs and Prophets*, p. 493

Maswali ya Moyoni: Unapotafakari Ebr. 4:12, unalionaje Neno la Mungu likiuchoma moyo wako mwenyewe? Je! Uliguswa na kitu fulani ulichosoma kwenye Neno la Mungu hivi karibuni? Je! Uliutendea kazi ule mguso au uliusukumia pembeni ushawishi wa Roho Mtakatifu? Msirikishe mtu fulani mawazo yako. Kisha omba kwamba, sisi kama watu, sio tu tulisikilize Neno na kulipenda Neno, bali pia tuweze kutafuta kuishi sawa sawa na Neno.

Taarifa ya Sifa: Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya video, mahubiri, semina za afya, na masomo mengine ambayo yametolewa na watu wa Mungu katika haya majuma machahce yaliyopita. Haya masomo mazuri na yenye uvuvio wa Roho Mtakatifu, kiuhalisia yamewabariki maelfu ya watu. Katikati ya zahama watu wa Mungu wanaangaza kwa utukufu wake.

Omba kwamba Mungu aweze kuizingatia ahadi yake ya Zaburi 91:7, kwamba “Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe.”

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea idara ya Kiadventista ya Chaplensia wanapoendelea kuwafariji wale wanaoteseka na wenye uhitaji.

- Ombea wale wanaoteswa kwa ajili ya imani katika maeneo ya Mashariki ya Kati na Asia. Omba kwamba wadumu kuwa imara na kuonesha upendo kwa watesaji wao.

- Endelea kuomba kwa ajili ya mipango mipya ya mkutano wa sesheni ya Konferensi Kuu itakayofanyika Mei 20-25, 2021, kule Indianapolis. Ombea kwamba mikutano ijazwe na mipango ya kiroho, inayolenga utume na kwamba Roho Mtakatifu atawale kikamilifu.

- Ombea kwa dhati umwagwaji wa Mvua ya Masika kwa Kanisa, ili ujumbe wa wokovu ufike pande zote za dunia na Yesu aweze kurudi.